

WALAKA WA VIJANA WA JESHI LA KUJENGA TAIFA

OP KIKWETE KWA MHE RAIS WA JAMHURI

YA MUUNGANO WA TANZANIA

DKT. JOHN POMBE MAGUFULI

Salamu kwako mheshimiwa rais wetu wa jamhuri ya muungano wa Tanzania na amri jeshi mkuu. Pia pongezi kwa juhudi zako nyingi katika kutekeleza majukumu yako ya kila siku katika kusimamia nchi vema na kila sekta kwa sasa imeimarika kiutendaji na kwa juhudi zako na msimamo wako ufanisi katika wizara na sekta zake unakwenda vizuri na hii sio jambo la kifichi kwa kila taifa linatambua sifa zako katika utendaji na usimamizi wa nchi hasa ukiangalia swala la kuinua uchumi wa taifa.

Sisi kama vijana askari wa jeshi la kujenga taifa tunatambua hilo na kutoa pongezi zetu nyingi kwako kwa juhudi na ufanisi mkubwa wa kusimamia Taifa vema, ukilinganisha na marais wanaofanya vizuri kwa bara la Afrika na dunia, wewe ni moja ya mfano wa marais wanaotenda vema kazi ya kusimamia Taifa lako baada ya kushika nyadhifa za kuwaongoza wananchi. Sisi vijana askari wa Jeshi la kujenga Taifa tunakupongeza sana kwa hayo yote na pia tunakuunga mkono kwa kila hatua na kuzisimamia juhudi na harakati zako za kuliendeleza taifa katika Nyanja zote.

Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu yako tunapenda utambue pia baadhi ya utekelezaji wa majukumu ya sekta nyingine ndani ya serikali yako jinsi wanavyo yasimamia na kuyatekeleza. Tumeona ni vema ufahamu na utupie jicho lako kwa mapana katika sekta ya ulinzi kupitia Jeshi la kujenga Taifa namna na jinsi ya uendeshaji na usimamizi wa majukumu kuwa hautekelezwi kwa kufuata misingi bora na mfumo wa malezi hasa katika fursa ya ajira inapotokea ndani ya jeshi hilo.

Mheshimiwa Rais hizi ni kelele za watoto wa wakulima, wanyonge na wachapakazi waliohudumu kwa miaka miwili na nusu wakifanya kazi nzito usiku na mchana za kulijenga na kuliimarisha Taifa bila kuchoka wala kinyongo, kazi zinazo simamiwa na maafisa wa Jeshi hilo, mafunzo tuliyopata kwa nje ama kwa tafasiri ya wakufunzi wetu wanaona yapo chini na huwenda wakaona ni kawaida, lakini Mheshimwa tunakuhakikishia vijana wako watanzania sisi tumejifunza mafunzo ya aina nyingi ndani ya Jeshi la kujenga Taifa.

Mbali na mafunzo ya Kijeshi ambayo huwenda wakufunzi wengi wenye dharau wanaweza kupuuza wakajua labda ni jambo la kawaida lakini kwetu ulinzi ndio uliotuleta JKT na ambao tumeutekeleza kwa juhudi kubwa, uzalishaji kwa kiwango cha hali ya juu ali kadharika manyanyaso ya wakufunzi kwa kiwango kisichoelezeka na tulivumilia kwakuwa tulikuwa ndani ya chombo kabla hatujarudishwa nyumbani, hivyo tumeona fursa ya kuzungumza yaliyo moyoni ni huu walaka wetu Mheshimwa rais utambue uchungu tulionao.

Mheshimiwa kama ilivyo ndani ya JKT watu kuwa na nidhamu, siri na uvumilivu kwa kuwa wawazi hatukupenda kuizungumzia JKT kwa nje lakini imetubidi tufanye hivyo huwenda sauti yetu ikasikika vema ndani na nje ya serikali yako. tunapenda kuomba kutambua masikitiko yetu na ombi letu katika kujali na kuliangalia swala tunalokuletea mbele yako.

Tupo katika wakati mgumu sana kwa sasa Mheshimiwa rais, tunaamini kwamba “JKT HAI AJIRI” sawa, lakini kunajambo ambalo linakera sana tena sana kwa nafsi zetu na kwa jinsi tulivyokaa humu ndani kwa kipindi kirefu tukifanyakazi za uzalishaji na ulinzi wa taifa lakini leo vijana askari wa Jeshi la Kujenga Taifa JKT Idadi 2050 tunalia kwa uchungu wa kurudishwa nyumbani tukiwa hatuna lolote, hatuna chochote. Uzalishaji mali ambao tumeona umefanyika hata cheti chake huwezi kwenda sehemu ukatafutia kazi, pili ulinzi tulioufanya hakuna sehemu ya kwenda kuufanyia zaidi ya kuwaweka vijana katika ushawishi mkubwa wa kuhitajika na vikundi vya kijasusi ili kwenda na kujiunga nao.

Sio vijana wote waliorudishwa nyumbani kuwa watakuwa na akili sawa ya kukaa na kutulia bila kujihusisha na mambo maovu kwa kuwa wamekata tamaa ukizingatia wametumia muda mwingi wakiwa JKT lakini hakuna wanalorudinalo mtaani zaidi ya kuwa anajua kutumia silaha na kwata pengine uzalishaji mali kwao sio nguzo muhimu wanayoweza kuitegemea wawapo nyumbani, kwani bila mitaji hakuna wanachoweza kukifanya. Mheshimwa tunapenda utambue pia mambo ambayo yamepelekea sisi vijana wa Oparesheni Kikwete 2015 – Dec 2017 kuzungumza kwa uchungu na kuona vema tukaandika walaka huu kwako Mheshimwa rais.

Swala la kuondolewa JKT bila hoja za msingi kwa kutugawa makundi mawili kati yetu tumeona wote tuliorudi nyumbani tumefanyiwa kitendo cha kikatili na ni kitendo cha unyanyasaji mkubwa sana na swala hili linatumiza sana vijana wako kwa kuwa fursa ya ajira kwetu ilikuwa ni nzuri kwa kipindi tulichokaa JKT, lakini mfumo tuliozungumza hapo mwanzo kwa sasa JKT haitumii kabisa jambo ambalo kwa miaka mitatu sasa vijana wamekuwa wakijazana katika makambi na hivyo kupelekea wimbi kubwa la maafisa wa Jeshi kutumia madaraka yao vibaya na kuligeuza Jeshi la Wananchi wa Tanzania na JKT kwa ujumla kuwa ni Jeshi la “wanajeshi” wenyewe na sio Jeshi la wananchi.

Tunasema hivyo kwakuwa vijana waliofanyiwa usaili mwaka 2015 Oparesheni Kikwete walikuwa 4890 na hadi kozi yetu inamalizika tulikuwa 4580 wengi walikata tamaa na kutoroka, wengine waliondoka kwa hiyari yao wenyewe, wengine walipata ajari na kufa (mf. Vijana wa JKT 821KJ Bulombora waliokufa kwa ajari ya gari la Jeshi wakiwa katika majukumu yao ya kikazi, wakipeleka chokaa mjini kuuzwa kigoma mjini.) lakini pia mheshimwa rais bila huruma na ukatili mkubwa vijana walionusulika katika ajali hiyo baadhi yao wakiwa na majeraha makubwa milini mwao nao wamebaki. Pia wapo waliopewa mimba na askari na wengine waliondoka kwa kurubuniwa na askari kuacha jeshi na kwenda kuolewa. Lakini hata baada ya idadi hiyo vijana wa Op kikwete walizidi kupungua kwa vijana 1800 kuchukuliwa kwenda Jeshi

la Magereza kuajiriwa, tukazidi kupungua zaidi tukijua hata Polisi, Jeshi la zima moto, Tanapa, Uhamiaji, Takukuru, JWTZ nk wangekuja na kutupunguza idadi yetu kama si kuimaliza makambini.

Lakini Hali imebadilika Mheshimwa Rais lile Jeshi la wananchi wa Tanzania limekuwa Jeshi la Wajeshi wenyewe kwa ukilitimba wa hali ya juu unaofanyika ndani ya jeshi, ndani yake unamlengo hasi wa ruhusa, ukabila na kujuana kiukoo na kifamilia (family friends) kutengeneza nafasi nyingi za ajira na kupewa watoto wa wanajeshi bila kutanguliza UZALENDO na kufuata mfumo wa kugawa nafasi hizo. Pengine hawajafuata mfumo wa kuajiri kama historia ya JKT katika fursa ya ajira na badala yake wameendelea kuyafanya hayo kwa mfumo ama muundo wa ajira za jeshini.

Tunaendelea kusikitika kwa kuwa vijana wenzetu ambao ni OP Magufuli wa mwaka 2016 -2017 ambao hawana hata vigezo vya kimkataba na hawajawahi kufanya hata usaili wa Jeshi wakiwa makambini lakini wamechukuliwa karibu asilimia 60% na kupelekwa kwenye ajira ya JWTZ na sasa wapo huko KIHANGAIKO NA OLJORO jambo ambalo ni kinyume na agizo lako ulilolitoa siku ya kuapisha Maafisa wapya wa JWTZ huko Arusha TMA ukiagiza ajira za jeshi zifuate utaratibu kwa kupewa nafasi vijana wa JKT hasa walio maliza mkataba wao. Hali kadharika wapo raia wametokea mtaani (wacheza ngoma, ngumi, mpira na riadha) wameajiriwa, wakati vipaji hivyo vipo ndani ya JKT na wamekuwa wakishiriki mashindano ya ndani na nje katika wilaya na mikoa nchini Tanzania wengine wamekuwa wakiimba katika ziara mbali mbali za viongozi wa Kitaifa. Mfa wewe mheshimiwa rais umekuwa ukiimbiwa na kuoneshwa na vikundi mbali mbali vya sanaa za maonesho kutoka JKT.

Lakini hakuna hata mmoja wao kati yetu sisi vijana wa JKT ambao wamekwenda katika ajira wakitokea katika vikundi hivyo, tupo nao mtaani mapaka sasa pengine ni watoto wenzetu wa masikini. Mheshimiwa rasi wale ambao hawana hata vigezo na wamepewa kipaumbele kwa sasa wameingizwa katika ajira hizo na wengine ni wale OP magufuli Mujibu wa sheria waliobakizwa Jeshini kama wa kujitolea nao wamekwenda kwenye ajira bila hata vigezo sawa na Op Magufuli.

Kimsingi Mheshimwa Rais vingetumika vigezo ambavyo huko nyuma vilikuwa vikitumika kwamba waliomaliza mkataba ndio huwa wakiipewa kipaumbele cha kwanza katika ajira kama zikitokea kabla ya Oparesheni nyingine. Lakini awamu hii licha ya kusubilia wenzetu wa Oparesheni Miaka 50 ya Muungano waliokaa miaka mitatu wamalizike kwanza makambini kwa kupata ajira na tulikuwa tukiomba hivyo na ikawa, kimsingi wote wamepata ajira awamu hii. Mheshimwa Rais lakini kwa awami hii tena baada ya wewe mwenyewe kutangaza ajira haikufanyika hivyo kati yetu Oparesheni Kikwete na Oparesheni Magufuli na inatumiza na kututia uzuni mkubwa na bila huruma mwisho wa siku tumerudishwa nyumbani bila kuelezwa chochote, inauma sana sana mheshimiwa Rais.

Hatusemi kuwa vijana wenzetu hawastaili kupata ajira la asha! Lakini wapate ajira kwa utaratibu kwani mfumo wa JKT kuajiri vijana (kama fursa ya ajira ikitokea) katika vyombo vya ulizi ndani ya Taifa hili ungefuatwa kwa Oparesheni Magufuli kusubilia kama sisi tulivyosubili na mkataba wetu ukaisha bila

ya Bogi la ajira kuwepo, ndivyo wangepanyiwa na wao vivyo hivyo kwani hata mkataba wao Oparesheni Magufuli bado hupo sana tu kwa sasa ni mwaka mmoja tu tokea wamejiunga na JKT na hivyo ingefika mwaka 2018 nao muda wao ungewadia kwani ndio kipindi cha wao kumaliza mkataba.

Mshemiwa Rais kimsingi vijana wako sisi watazania tumepitia katika changamoto nyingi sana ndani ya Jeshi la kujenga Taifa na mambo ya msingi tumejifunza lakini sasa tunarudishwa nyumbani na elimu zetu na ujuzi wetu, huwenda wale waliopata ajira ni muhimu na wanabahati kubwa sana ya kutengenezwa na hawa binadamu na hivyo sisi tulio wengi watoto wa masikini tunaonekana hatuna bahati na hatustaili kufanya kazi ndani ya serikali na jeshi kwa ujumla.

Mheshimiwa Rais hatukustaili kuandika waraka huu kwa uwazi kiasi hiki tukijua kuwa si vema kuzungumza hivi na ni kiunyume na utaratibu na kanuzi za maadili ya kijeshi, lakini Mheshimiwa kwa maumivu na uchungu mkubwa tulioupitia na manyanyaso makubwa tunayofanyiwa sisi vijana wa JKT kimsingi tumeshindwa kuvumilia maana muda na wakati tuliopitia na kitendo tunachofanyiwa kimsingi hatukustaili kabisa mheshimiwa rais. Kwani hata sisi ni watazania na ajira ni haki yetu sote kikatiba, lakini kwa nini ubaguzi huu na kwa nini iwe hivi kwetu sisi, na kwa nini asilimia kubwa ifanyike kwa watoto wa masikini?

Mheshimiwa rais tunapenda utambue kuwa kuna athari kubwa sana zitakazotokea kwa sisi vijana wa Oparesheni Kikwete zaidi ya 2000 kurudi nyumbani, miongoni mwa athari hizo zinalenga Uchumi, Kiasa na kijamii.

Kiuchumi

Kuongezeka kwa wimbi la vijana tegemezi katika jamii.

Kitendo cha vijana kurudi nyumbani tukiwa na ujuzi bila mtaji ama ajira inapelekea vijana wengi kwenda kuwa tegemezi kwa familia zao jambo ambalo litapelekea uchumi wa familia kudorora.

b. Matumizi mabaya ya fedha za serikali.

Kupunguza mzunguko wa kiuchumi ambao ungechangiwa na vijana tuliorudishwa nyumbani tukiwa hatuna hata mtaji kutokana na mafunzo tuliopata kwa ghalama nyingi za serikali ambazo leo zinaonekana kuwa patupu (horrible) na feza za serikali zimepotea bure bila malengo kutimbia. Pengine vijana wangepata mtaji ama ajira katika jamii mzunguko wa kiuchumi katika familia zetu na Taifa letu kwa ujumla.

c. Kuongezeka kwa ombwe kubwa la vijana kutokuwa na ajira.

Kila mwaka vijana watazania wanamaliza vyuo na pia sisi vijana Oparesheni Kikwete tunarudi mwaka huu pekee tunarudishwa nyumbani na fursa na kwa sasa kuna fursa chache za ajira binafsi na za serikali hali hii inaonesha dhahiri kuwa mtaani tunaenda kuwa na wimbi kubwa la vijana wenye taaluma wasio na ajira na kuchangia kuzorotesha uchumi wa familia na Taifa kwa ujumla.